Kwako bibi :

Masomo ya juu siyo mlango wa ukahaba !

Mwananchi Lubunga Bya 'Ombe ambaye ni mwandishi wetu maalum kutoka chuo cha upashaji wa habari (ISTI) huko Kinshasa azungumza na akina dada wanaosoma katika Univasti na vyuo vikuu. Dada hao wazani kuwa ukahaba ndio njia ya kujitajirisha ao kujipatia "lwa sombe". Watumia vibaya uhuru walioachiwa na wazazi wao kwa kuuza (vendre) mwili wao kama kalanga sokoni.

Dada mpenzi, ulipomaliza masomo ya sekondari, ulifikiri kama umeumaliza mwendo, na jamaa lote lilifurahi sana. Wakati ule rafiki zako wamoja walijiharakisha kuolewa, lakini wewe uliamua kuendelea na majifunzo. Ulifanya vizuri sana. Lakini sasa umesahau ya kuwa nia yako kubwa ni kumaliza masomo na kujipatia cheti cha masomo ya juu. Hivi sasa unaifuata njia ya ukahaba (ndumba, mbaraga) kama huo ndio usirimu.

Umesahau pia kama wazazi wanakutegemea sana, wakingoja hapo utakapomaliza. Jamaa nzima litasifiwa. Pahali pa kusoma vitabu na mabuku yako, unapoteza wakati mwingi ukizunguuka kwenye mahoteli pamoja na mabwana sukari wenye magari makubwa makubwa. Haujui kama nia ya mabwana hao ni kufyonza uzuri wako na kisha kuharibu majifunzo yako kusudi uchekelewe popote pamoja na wabinti wanaoʼizaraulisha ? Utaniambia eti hiyo ni njia ya kutafuta "lwa sombe", kwani huko kwenye "home" unakokaa maisha yamekuwa magumu. Usidanganyike, dada mpenzi. Maisha ya siku hizi ni magumu kwa watu wote, wanafunzi binti kama vile wavulana. Basi mwenendo wako hauwaheshimishe wazazi wako. Hata na wewe mwenyewe umepoteza pendekezo lako mbele ya watu wote. Ungevumilia njaa kwa ʼaka michache inayokukilia ili upate kumaliza. Na utaona kama taabu yote ya kianafunzi ni ya saa ao siku chache.

Ninajua kama unafuata mfano wa yule mwenzako ambaye alijinunulia mavazi na viherena kwa feza anazopewa na mabwana wengi. Kufuata mifano mibaya si vema kwako binti uliyeadibishwa vizuri na mwenye elimu. Unasahau kama utakapomaliza masomo yako utapata feza za kutosha na kununua vyote utakavyotamani ? Yafuate kwanza masomo na mambo mengine yatakuja baadaye.

Lazima tu usiache dini kama vile wazazi walivyotufundisha. Siku nyingine ulinielez[...] mwalimu alikush[...] kulala naye kub[...] baadaye akupati[...] Mwalimu huyo mzee[...] danganye, kwani [...] na watoto wengi [...] nia ya kujipati[...] kwa wenzake, kwa[...] mwaka anayo tabi[...] mbaya ya kutongoza[...] nti masomoni. U[...] eti utakosa alama[...] ni utakapokataa[...] kunako mahoteli[...] kualika. Jikaze[...] majifunzo ya si[...] siku, utajionea m[...] mazuri. Ninatara[...] ta jibu lako kw[...] hii, wewe dada un[...] kwenye "home" [...] ya juu mahali p[...] nikitumaini kuwa[...] kiri mengi juu ya[...] haya ninayokuandi[...]

LUBUNGA BYA'OM[...]

Mwananchi Edjonga awatetemesha walinda Feza

Siku hizi, walinda feza ambao wanayo tabiya mbaya ya kuchopoa feza za serikali watiliwa lisani pembeni. Wanaposikia kuwa makamu wa liwali wa jimbo ambaye pia ni kiongozi wa kamati ya uchunguzi wa mishahara ya wafanyakazi wa serikali pamoja na ujumbe wake atafika kuwachungua wanaanza kutetemeka kama majani mbele ya baridi.

Kisha uchunguzi alioufanya huko Uvira na hapa mjini Bukavu, mwananchi Endjonga pamoja na wasaidizi wake walivumbua kuwa walinda feza watunga daftari ya majina ya watumishi wa uwongo kusudi ya kupokonya feza wakizani kuwa serikali yetu ni nchi ya wajinga.

Kufuatana na uchunguzi huo wa Uvira na Bukavu, zaïre yapata 800.000 ambazo zilitaka kupekenywa na wale wala pupa ziliweza kurudishwa katika sanduku ya serikali. Maelfu hayo yote ya feza yaligunduliwa tu kwa mwezi wa pili uliopita. Kwa ngambo yetu, twaona wazi kuwa jamaa hao ambao hawakukuwa na matatizo yoyote ya feza ndio msinji wa magumu ya feza inayoikabili nchi yetu. Wale wanao wafahamu vema wasema kuwa feza hizo walikuwa wakizitumia kila mara kwa kununua magari ya bei ghali, kuhonga wanawake, kula chakula kizuri nyumbani kwao, kulewa pombe bila kiasi na kutengeneza vilabu vya pombe. Miongoni mwa wale walionaswa hapa Bukavu na Uvira twaweza kutaja majina ya wala pupa: Nsila wi Mubuemu, Milambo wa Munga pamoja na Lokemba Atakone. Jamaa hao wapatikana mbele ya waamzi ambako wasamba makosa yao wakijuta ile malofu ya aina ya "wisky" (walikuwa wamekwisha kuapa kunywa primus wakisema eti hiyo ni pombe ya washenzi) na makahaba wao wote wamewakimbia.

Kufuatana na habari tuliyopata kutoka tawi la shirika la upashaji wa habari nchini kwa kifupi AZAP huko Goma, inasemekana kuwa alipofika huko Goma, mwananchi Endjonga na wasadidizi wake waligundua kuwa walinda feza wa huko nao ni wevi. Ni hivi aliomba kwa waamzi wawasambishe na wawapatie malipizi makali kwa kuwatolea mfano wale wengine ambao wapendelea kupekenya feza za serikali kama kalanga wakizani kuwa bakora ya mapinduzi imekwisha kuvunjika. Ni hivi zaire 30.000 zimerudishwa katika sanduku ya serikali.

Ujumbe huo wa kuchungua malipo ya wafanya kazi wa serikali ulijielekeza Kindu, mji mkuu wa wilaya ya Maniema kusudi ya kuendelea na kazi zake. Wasafiri kutoka Maniema huhakikisha kuwa walinda feza wa huko hawanywe tena maji na "loho balili". Hawaonekani tena katika vilabu vya pombe kama ilivyokuwa hapo hawali zoezi yao. Wengine huhakikisha kuwa huko kutatoka habari ya kuwatupa gerezani wale wanaopendelea kugeuza sanduku la serikali kama vile mfuko wao.

Kaboyi Habimana.

JUA

Gazeti la Kivu

Kinshasa Munamo tarehe 15 aprili 1985

* Zitaanzishwa kazi za kamati kuu ya Cham[a]

Habari zinazoaminika kutoka Kinshasa, mji mkuu wa Jamhuri ya Zaïre zaeleza kuwa kamiti kuu ya Chama chetu cha Mapinduzi (comité central du MPR) itafungua milango yake siku ya kwanza tarehe 15 Aprili ijayo.

Ni katibu wa kilele wa kiungo hicho cha Chama, akina mama Lessendjina ndiye alitoa habari hiyo kwenyi ofisi ya redio na televisheni huko Kinshasa, kisha mkusanyo wao na Baba wa taifa, mheshimiwa Mobutu Sese Seko. Mkusanyo huo uliendeshwe huko Gbadolite (Ekwatori)

Mama Lessenjina alieleza kuwa kazi hizo ambazo zilipashwa kuanzishwa tangu tarehe 1 Aprili zilipangwa mnamo tarehe 15 Aprili kutokana na programa ya kazi iliyopangwa na Baba wa Taifa mwenyewe.

Mbele ya kuanza kazi hizo, wanamemba wa Chama chetu cha Mapinduzi watapewa mwanga kuhusu siasa ya Chama chetu cha Mapinduzi. Mafundisho hayo yataanzishwa tangu tarehe 13 mpaka 14 Aprili 1985.

Kwa ngambo yake, bunge la Taifa (Conseil législatif) lilianzisha kazi zake tangu [...] moja Aprili iliyopit[a] nako jumba la [...] (Palais du peuple) Kinshasa.

Alipochukua [...] mwananchi Kasongo [...] kunji, kiongozi wa [...] la Taifa alieleza [...] kiungo anachoongoza [...] tafuata njia ya Bab[a] Taifa kusudi ya ku[...] namna ya kuim[...] maisha ya wakaaji [...] wa miaka saba an[...] ka kupewa kwa ku[...] jamhuri ya Zaïre.

Kaboyi Habima[na]

Tuzungummze

Adabu nyumbani mwa Sinema

Tunaendelea kuchapa maandishi ya mwananchi Kimengele Kimode kuhusu namna tunavyoaminika kuishi katika makundi ya watu. Katika mistari ifuatayo, atiya mkazo juu ya adabu nyumbani mwa sinema.

Katika Afrika ya kisasa watu karibu wote wajua sinema vizuri sana na hupenda kuiona mara nyingi. Kwa kweli sinema, zaidi ya kutufurahisha, inatuelimisha na kutupatia maarifa mengi ikitujulisha mambo yanayotendeka barani zingine ingawa hatujafikamo!

Vema zaidi wataalam walivumbua televizio. Kwa msaada wa televizio twaweza kuona na kusikia mambo ya pengine ginsi yanayotendeka kule, kwa wakati ule ule yanapotendeka.

Lakini sinema kama vile televizio ingawa vinavyo mafaa mengi sana katika maisha ya ujamii vyaweza kuwa na hasara kubwa mno hasa kwa yale yenyi kuhusu malezi ya watoto vijana.

Katika nyumba ya sinema angalia na fwata kwa angalisho picha, maandiko na tosha[...] katika kufwatana k[...] cha na kuambata[...] vitendo. Usicheke[...] kumzuru jirani wa[...] yame kwa kuonya r[...] ko ama kujulisha[...] lako kwa kitendo [...] Usivute nyumbani [...] nema. Nyumba zile[...] desturi, hazina d[...] na hata ingaliku[...] funguliwi wakati[...] Kumbe ukivuta ut[...] hewa na mara u[...] jirani. Pia kuna [...] ya kuunguza jengo[...]

Kwa namna yako [...] sangaa, ya kuche[...] kufurahi au ya [...] huhukumu malezi [...] ta.

(Itaende[lea])

Kimengele Kim[ode]